**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**IMEWASILISHWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2025**


Mhe. Omar Said Shaaban
Waziri wa Biashara na
Maendeleo ya Viwanda


Ndg. Fatma M. Khamis
Katibu Mkuu
Wizara ya Biashara na
Maendeleo ya Viwanda


Dkt. Said S. Mzee
Naibu Katibu Mkuu
Wizara ya Biashara na
Maendeleo ya Viwanda


Ndg. Ali S. Abeid
Afisa Mdhamini
WBMV-Pemba


Ndg. Kassim S. Ally
Mkurugenzi
DAP


Ndg. Jamila Sh. Salum
Mkurugenzi
DPPR


Ndg. Khamis A. Shauri
Mkurugenzi
DTM


Dkt. Abdulla R. Abdulla
Mkurugenzi
DID


Ndg. Yussuf Nassor Majid
Mkurugenzi Mkuu
ZBS


Ndg. Khamis J. Khamis
Mkurugenzi Mtendaji
BPRA


Ndg. Soud S. Ally
Mkurugenzi Muendeshaji
ZSTC


Ndg. Mohammed S.
Mohammed
Mkurugenzi Mkuu-ZFCC


Dkt. Masoud R. Mohammed
Mkurugenzi Mkuu
ZASCO


Ndg. Mohammed M. Simai
Mkurugenzi Mkuu
ZAWEMA


Ndg. Mtumwa Kh. Ameir
Afisa Mtendaji Mkuu
COSOZA


Ndg. Salmin Sh. Khatib
Katibu Mtendaji
ZNBC


Ndg. Fatma Gh. Haji
Mrajis
ZFCT


Dkt. R'dhan Kh Ramadhan
Kaimu Katibu Mtendaji
BLRA

# YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1
2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA ............... 2
3.0 MWENENDO WA BIASHARA .............................. 4
3.0.1Hali ya Uchumi na Biashara Duniani. ............... 4
3.0.2 Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi Nyengine Duniani. ............................................ 5
3.0.3 Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. ................................................................ 6
3.0.4. Hali ya Chakula na Bei Katika Soko la Zanzibar ............................................................ 6
4.0 MWENENDO WA VIWANDA ............................... 7
5.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA ................................................ 9
5.0.1 Ukusanyaji wa Mapato..................................... 9
5.0.2 Mafanikio ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda............................................. 9
5.0.3 Changamoto za Wizara na Njia za Utatuzi. ..... 11
6.0.MATUMIZI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI, 2025 ................................. 13
7.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI, 2025....... 13
8.0 MASHIRIKIANO NA MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA (TANTRADE) .................. 37
9.0UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOSIMAMIWANA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024-MACHI 2025. ................. 38

9.0.1Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda .......... 39
9.0.2Mradi wa Kuyaendeleza Maeneo ya Maonesho ya Biashara Dimani.......... 41
9.0.3 Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar. .......... 42
10.0 MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (4) HADI MACHI 2025.......... 44
10.0.1 Kuimarisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda 44
10.0.2 Kuimarika kwa sekta ya Biashara .......... 46
11.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI AMBAZO HAZIPOKEI RUZUKU SERIKALINI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 - MACHI 2025.......... 51
11.0.1 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) .......... 51
11.0.2 WAKALA WA USAJILI BIASHARA NA MALI ZANZIBAR (BPRA) .......... 54
11.0.3 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) .......... 57
11.0.4 KAMPUNI YA MWANI (ZASCO) .......... 60
12.0 MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.......... 62
12.0.1 Vipaumbele Vya Wizara Na Taasisi Zake Kwa Mwaka 2025-2026. .......... 62
12.0.2 Sekta Ya Viwanda .......... 62
12.0.3 Sekta ya Biashara.......... 63
12.0.4 Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma .......... 64
12.0.5 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) .......... 65

12.0.6 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA) .......... 66
12.0.7 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) .......... 66
12.0.8 KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR (ZASCO) .......... 67
13.0 MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/2026 .......... 67
14.0 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .......... 71
14.0.1 MAPATO YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/2026 .......... 71
14.0.2 MATUMIZI KWA MWAKA 2025/2026 .......... 72
15.0 HITIMISHO .......... 74
VIAMBATANISHO .......... 77

**HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, kwa kuibariki nchi yetu kuendelea kuwa na amani na utulivu na kutuwezesha kufika hapa leo katika Baraza lako Tukufu tukiwa na uzima na afya ili tuweze kuwasilisha bajeti hii. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa uwezo wa kuyasimamia na kuyatekeleza majukumu yetu kwa faida ya Taifa letu.

2. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mkutufu napenda kuchukua nafasi hii ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi kwa imani yake kwangu ya kunipa dhamana ya kusimamia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda tangu aliponiteua. Nampongeza pia kwa jitihada zake alizozichukua na anazoendelea kuzichukua katika kuwaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo na jitihada zake kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinaendelea kutawala katika visiwa vyetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa namna anavyompa mashirikiano Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kuiletea maendeleo Zanzibar na kuhakikisha kuwa Haki za wananchi zinapatikana ili Nchi yetu iwe na amani ya kudumu. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** kwa uamuzi wake wa kuchukua fomu ya kugombea Uraisi wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT Wazalendo. Namtakia kila la kheri.

4. **Mheshimiwa Spika,** Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** kwa jitihada zake za dhati anazozichukua za kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile kwa kutupa miongozo, maelekezo na michango yake katika maendeleo ya nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa mashirikiano makubwa, michango na ushauri mliotupatia kwenye Wizara katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024-2025.

6. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuchukua nafasi hii kwa umuhimu wake kuishukuru Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inayoongozwa na Mwenyekiti

wake Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini. Aidha, nawapongeza wajumbe wa Kamati ambao ni Mheshimwa Hussein Ibrahim Makungu, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wake akiwemo Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Ali Suleiman, Mheshimiwa Mihayo Juma Suleiman, Mheshimiwa Said Saleh Salim, Mheshimiwa Saada Ramadhan Mwendwa na Mheshimiwa Suleiman Makame Ali pamoja na Makatibu wao. Hakika maoni na ushauri ambao Kamati hii ilikuwa ikitupatia yamesaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara iliyojipangia. Tunapohitimisha muda wa Uhai wa Baraza hili, nawatakia kila la kheri katika Uchaguzi ujao.

7. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile nawapongeza Wafanyabiashara, Wawekezaji katika Viwanda na Wazalishaji kwa jitihada zao za kuiunga mkono Serikali kwa kuendelea kuibakisha mitaji yao ya fedha na Mali katika kukuza Biashara na Uzalishaji hapa Nchini. Ninawaahidi kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuweka mazingira mazuri zaidi ya wao kukuza Biashara na Uwekezaji wao kama ilivyo ahadi yetu kwao.

8. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya Shukrani na maelezo hayo ya awali, naomba kuanza Hotuba hii kwa kuwasilisha Muundo wa Wizara, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikijumuisha mafanikio,

changamoto na njia za utatuzi wake, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hatimae kuwasilisha mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## 2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imeundwa na Idara nne (4) ambazo ni Uendeshaji na Utumishi, Mipango, Sera na Utafiti, Maendeleo ya Viwanda, Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na Afisi Kuu Pemba. Aidha, inasimamia Taasisi 10 ambazo ni ZFCC, ZFCT, ZAWEMA, ZNBC, BLRA, COSOZA, ZBS, ZSTC, BPRA na ZASCO na inatekeleza majukumu makuu yafuatayo-

i. Kuandaa na kusimamia Mipango, Sera, Sheria na Tafiti zinazohusiana na sekta zilizo chini ya Wizara;

ii. Kusimamia kuwepo kwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji;

iii. Kusimamia na kuimarisha mazingira mazuri ya ufanyaji Biashara;

iv. Kuhakikisha bidhaa na huduma zinazozalishwa zinakidhi viwango vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

v. Kuhakikisha uwepo wa masoko kwa bidhaa za ndani katika masoko ya Nje ya nchi;

vi. Kusimamia na kukuza maendeleo ya Viwanda;

vii. Kusimamia shughuli za usajili wa biashara na mali;

viii. Kusimamia usawa wa Vipimo katika ushindani wa kibiashara;

ix. Kusimamia utoaji wa leseni ili kupunguza urasimu na kurahisisha utoaji wa leseni na vibali;

x. Kusimamia maendeleo ya karafuu kwa kununua na kuuza karafuu nje ya nchi;

xi. Kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa zinazotokana na maamuzi ya Tume ya Ushindani Halali wa Biashara pamoja na mamlaka nyengine za udhibiti;

xii. Kuratibu na kusimamia Rasilimali Watu, Mipango na Utawala katika Kampuni ya Mwani;

xiii. Kukuza mahusiano kati ya Sekta Binafsi na Serikali; na

xiv. Kusajili, kukusanya na kugawa mirabaha kwa wamiliki husika wa haki miliki waliosajiliwa.

## 3.0 MWENENDO WA BIASHARA

### 3.0.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani.

**10**. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Ripoti ya Biashara pamoja na Takwimu Duniani mwezi Machi,2025 (Global Trade Outlook and Statistics) Mwenendo wa biashara Duniani kwa kipindi cha mwaka 2024 umefikia dola za Kimarekani 33 trilioni sawa na ongezeko la asilimia 3.7 (dola za Kimarekani 1.2 trilioni) ikilinganishwa na mwaka 2023 ambapo hali ya biashara ilikuwa dola za Kimarekani 31.8 trilioni. Ongezeko hili limechangiwa zaidi na biashara ya huduma kwa wastani wa dola za Kimarekani bilioni 700 sawa na asilimia 9.0 na kwa upande wa biashara ya bidhaa imechangia wastani wa dola za Kimarekani bilioni 500 sawa na asilimia 2.0

**11.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2024 usafirishaji duniani umeshuka kwa asilimia 4.3 na kufikia dola za kimarekani 23.8 trilioni kutoka dola za kimarekani 29.3 mwaka 2023. Hali hii imetokana na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa kwa nchi zinazoendelea kwa asilimia 6.2, nchi zilizoendelea kwa asilimia 2.8 na Afrika kwa asilimia 9.8 kwa mwaka huu. Kwa upande wa uagiziaji biashara Duniani kwa mwaka 2024 hali ya biashara imekua ikilinganishwa na mwaka 2023.

### 3.0.2 Biashara Kati ya Zanzibar na Nchi Nyengine Duniani.

12. **Mheshimiwa Spika,** Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji wa bidhaa nje umepelekea hali ya biashara kwa ujumla kuimarika, ambapo kwa mwaka 2024 Zanzibar ilifanya biashara yenye thamani ya Shilingi bilioni 1,825.5 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1,611.1 kwa mwaka 2023 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Bidhaa zilizosafirishwa kwenda nje ya Nchi ni pamoja na karafuu, vitenge, khanga, mwani, mazao ya baharini, vyuma chakavu, makapi ya ngano na ngozi za n'gombe na bidhaa zilizoagizwa ni bidhaa za chakula, dawa pamoja na vipuri vya magari.

13. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 105.28 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 109.26 mwaka 2023. Kiwango hicho cha usafirishaji kimepungua kwa asilimia 3.6 na hii imetokana na usafirishaji mdogo wa karafuu na bidhaa ya mwani. Bidhaa hizo zilisafirishwa katika masoko ya Singapore, Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Indonesia, India na Denmark.

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1,649.26 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thanami ya Shilingi

bilioni 1,501.87 kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Bidhaa ambazo Zanzibar imeagiza kutoka nchi za nje ni pamoja na mafuta, bidhaa za Viwandani, vyombo vya usafiri, nguo na bidhaa za chakula. Aidha, Zanzibar imeagiza bidhaa kwa wingi kutoka nchi za Falme za Kiarabu, China, India, Pakistani, Brazil, Uturuki, na Vietnam.

### 3.0.3 Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.

15. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa usafirishaji Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kipindi cha mwaka 2024, Zanzibar ilisafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara zenye thamani ya Shilingi bilioni 106.32 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 95.72 zilizosafirishwa mwaka 2023. Miongoni mwa bidhaa zilizosafirishwa kwenda Tanzania Bara ni pamoja na chuma chakavu, mafuta ya kupikia, mchele wa basmati na bidhaa nyengine za vyakula vya makopo. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2024, Zanzibar iliagiza kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 382.51 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 431.54 kwa mwaka 2023.

### 3.0.4. Hali ya Chakula na Bei Katika Soko la Zanzibar

16. **Mheshimiwa Spika,** Hali ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula hapa Nchini inaendelea kuridhisha na vyakula vyote muhimu vinaendelea

kupatikana bila ya usumbufu. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya Tani 24,746.08 za Mchele, Tani 18,708.02 za Sukari, Tani 705.50 za Unga wa ngano na Tani 102,207.71 za Mafuta ya kula ziliingizwa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani. Bidhaa hizo zinatoka katika Nchi za India, Brazil, Uturuki, Pakistani, na Vietnam. Aidha, uzalishaji wa ndani uliendelea kwa bidhaa za unga wa ngano ambao unazalishwa na kiwanda cha Zanzibar Milling kilichopo Mtoni. Takwimu zinaonesha jumla ya Tani 56,723.76 za unga wa ngano na Tani 7,900 za Sukari zilizalishwa nchini kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025. Taarifa za uwepo wa bidhaa zinaonekana katika **Kiambatanisho Nambari 1.**

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa bei za bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, unga wa ngano, sukari na mafuta ya kupikia katika masoko ya ndani zimekuwa tulivu kama ilivyokuwa kwa kipindi kilichopita cha mwaka 2023/2024. Hali hii imetokana na Wizara kusimamia hali ya ushindani halali wa bei katika soko, pamoja na kufuatilia bei elekezi kwa bidhaa hizi muhimu kwa maisha ya wananchi. Bei za bidhaa muhimu zinaonekana katika **Kiambatanisho Nambari 2.**

## 4.0. MWENENDO WA VIWANDA

18. **Mheshimiwa Spika,** Mchango wa sekta ya Viwanda katika pato la Taifa (GDP), umeongezeka kutoka asilimia 19.4 kwa mwaka 2022/2023 hadi asilimia

20.8 kwa mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo la asilimia 1.4 limetokana na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuwekeza miradi mikubwa ya ujenzi ambayo imepelekea kukua kwa sekta hiyo. Aidha; kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vikubwa vilivyopo ambavyo pamoja na kuanzishwa kwa viwanda vipya 25 vinavyojishughulisha na uzalishaji wa mafuta ya majani, karafuu korosho, maji ya kunywa vipodozi pamoja na viwanda vinavyotengeneza mabomba ya maji, boti za uvuvi, nguo na viatu, samani vifaa vya ujenzi, vifaa vya umeme, matangi ya maji na mabati kumechangia matokeo Chanya kwenye sekta ya viwanda katika kipindi hiki.

19. **Mheshimiwa Spika,** Uzalishaji katika viwanda vikubwa umeendelea kuimarika kwa upande wa Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation (ZMCL) kimezalisha jumla ya tani 56,723.76 za unga wa ngano kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikilinganishwa na tani 49,355.38 kwa mwaka 2023/2024 ambao ni sawa na ongezeko la asilimia 13.16.

20. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha sukari Mahonda kimepanga kuzalisha tani 9,000 za sukari kwa mwaka 2024/2025 ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi 2025 kiwanda hicho kimeweza kuzalisha tani 7,900 za sukari na lita 1,000,000 za spiriti, ukilinganisha na tani 8,700 za sukari na lita 800,000 za spiriti kwa mwaka 2023/2024.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA

### 5.0.1 Ukusanyaji wa Mapato

21. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 1.94** kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi bilioni 1.50.** Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi bilioni 1.20** zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya makusanyo kwa miezi tisa (9). Mchanganuo wa mapato kwa ujumla unaonekana katika **Kiambatanisho Nambari 3.**

### 5.0.2 Mafanikio ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

22. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami pamoja na miundombinu ya maji kwenye eneo lote la ekari 173, kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa usafishaji wa maji pamoja na kuweka vituo saba (7) vya kupokea maji wakati litakapotokea janga la moto katika eneo lote la viwanda Dunga Zuze, Wilaya ya Kati Unguja. Aidha, uimarishaji wa

ukumbi wa mikutano na ujenzi wa miundo mbinu ya vyoo katika viwanja vya maonesho umefanyika; Wizara imekamilisha Sera ya Biashara ya Mwaka 2024 pamoja na Ripoti ya Tathmini ya Mazingira ya Biashara ya mwaka 2025 ambapo Sera na Ripoti hizi zinalenga kutatua vikwazo katika ufanyaji Biashara na Uwekezaji nchini na Wizara imeweza kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo usajili wa biashara na mali kufanyika ndani ya masaa 24 badala ya siku tatu (3).

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kupata ithibati katika Maabara mbili (2) ya mafuta ya nishati na Maabara ya chakula na Kemikali; Wizara imenunua wastani wa tani 824.6 za Mwani zikiwemo tani 619.5 ni mwani aina ya "Spinosum", tani 48.6 mwani aina ya "Cottonii" na tani 198.2 za mwani aina ya Ulva kutoka kwa wananchi na imeuza tani 188 za Mwani mkavu nchini Vietnam na China na imenunua tani 412.4 za karafuu kwa Shilingi bilioni 6.24 na makonyo tani 5.9 za makonyo kwa Shilingi milioni 8.85 kutoka kwa wananchi pamoja na kuwapatia wananchi miche 32,000. Vile vile Wizara imefanikiwa kuandaa majukwaa mawili (2) ya Biashara ambayo yalilenga kutatua changamoto za ufanyaji biashara Zanzibar pamoja na Wizara imezisimamia Mamlaka za utoaji leseni 57 kwa kutumia mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma sambamba na Malipo ya leseni na vibali kulipwa kupitia Benki.

### 5.0.3 Changamoto za Wizara na Njia za Utatuzi.

**24. Mheshimiwa Spika,** Changamoto zinazoikabili Wizara ni pamoja na: -

i. Upungufu wa vifaa vya kufanyia kazi ikiwemo usafiri ambapo hupelekea kutokutekeleza shughuli zilizopangwa kwa wakati na ufanisi;

ii. Uhaba wa wataalamu kwa Taasisi ya Viwango na Kampuni ya Mwani;

iii. Uelewa mdogo wa madaraja ya karafuu kwa wakulima ni changamoto ambayo inaikabili Shirika la Biashara Zanzibar;

iv. Kukinzana na kutoendana na Sheria zilizoanzisha Mamlaka za Udhibiti na Baraza la Ushindani Halali wa Biashara katika vipengele vya ukataji wa Rufaa, jambo linalopelekea ugumu wa kutekeleza majukumu ya Baraza kwa mujibu wa Sheria;

v. Ukosefu wa mfumo wa Usajili wa moja kwa moja (online) wa uombaji na utoaji leseni kwa wamiliki wengi wa hakimiliki na watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara na kukosa kukusanya kiwango kikubwa;

vi. Kutotumika kwa Sheria wa Usajili ya Amana kwa mali zinazohamishika; na

vii. Uelewa mdogo wa Usajili wa Mali Bunifu kwa upande wa Wazanzibar.

25. **Mheshimiwa Spika,** Njia za utatuzi wa changamoto hizo kwa Wizara katika ukusanyaji wa mapato ni pamoja na: -

i. Wizara imefanya mazingatio ya kutosha kwa bajeti ya mwaka 2025/2026 kuhusu vifaa vya kutendea kazi;

ii. Wizara inaendelea na jitihada za kupata watendaji kwa mujibu wa Muundo wa Taasisi;

iii. Shirika la Biashara la Taifa linaendelea kuwapatia elimu wakulima kwa lengo la kuwaelimisha juu ya utunzaji bora wa karafuu na kufanikisha kupata daraja bora wakati wa uuzaji;

iv. Wizara inaendelea kutoa uelewa pamoja na kukaa na Mamlaka za Udhibiti kwa ajili ya kuhakikisha vipengele vya ukataji wa Rufaa husika vinafanyiwa marekebisho katika Mamlaka hizo;

v. Wizara inaendelea na taratibu za kupata mfumo wa usajili wa moja kwa moja na mfumo wa leseni ambapo mifumo hii itawezesha kurahisisha usajili wa wamiliki wote na kuwezesha ofisi kufikia maeneo mengi ya watumiaji wa hakimiliki kibiashara na kukusanya mapato ya mirabaha kwa kiwango kikubwa;

vi. Wizara kipitia BPRA, inaendelea kuelimisha taasisi za kifedha (benki) na watu binafsi wenye uwezo wa kifedha; na

vii. Wizara inaendele kutoa elimu kwa jamii kwa kuweza kusajili kazi zao kupitia vyombo mbali mbali ili kuzipa ulinzi kisheria kazi hiyo.

## 6.0. MATUMIZI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI, 2025

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi bilioni 60.28** kwa ajili ya kutekeleza programu zake. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025 Wizara ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 58.03,** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 18.40** sawa na **asilimia 31.7** ya makadirio ya miezi tisa zilipatikana ambapo Wizara ilipokea mgao wa fedha za matumizi kwa miezi minne (4) ya Agosti, Septemba, Disemba na Machi. Kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi bilioni 2.05** ziliingizwa kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 12.88** kwa ajili ya kazi za maendeleo na **Shilingi bilioni 3.48** kwa kazi za kawaida. Mchanganuo wa matumizi hayo unaonekana katika **Kiambatanisho Nambari 4.**

## 7.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI, 2025

27. **Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda yanatekelezwa kupitia programu kuu tatu ambazo ni Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na

Maendeleo ya Viwanda; Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali na Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara. Programu hizo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara za Wizara, Afisi Kuu Pemba pamoja na Taasisi zake ikiwemo ZFCC, BLRA, ZNBC, ZFCT, COSOZA, na ZAWEMA, ambapo utekelezaji wa programu hizo ni kama ifuatavyo: -

**PR0101:Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.**

**28. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kutoa huduma za Kiofisi kwa ufanisi na ustawi wa sekta ya Biashara na Viwanda. Programu hii imegawika katika Programu Ndogo tatu (3) kama ifuatayo:-

i. Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara.

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.

iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

**29. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 3.86 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi, 2025, Programu hii ilipangiwa Shilingi bilioni 2.98

na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi bilioni 2.50 zimeingizwa sawa na asilimia 83.9 kwa ajili ya kutekeleza programu hii. Utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo: -

**SR010101: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

**30. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina jukumu la kusimamia rasilimali watu, ununuzi wa vifaa vya Ofisi na kuratibu mikutano ya majadiliano ya biashara na viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

i. Wafanyakazi 14 wamepatiwa mafunzo wakiwemo wafanyakazi wanane (8) wanawake na wanaume sits (6), ikiwemo mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya kwanza kwa wafanyakazi saba (7) katika fani za Sheria, Uchumi, Mipango, Utawala na Uandishi wa Habari. Aidha wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utawala, Katibu Muhtasi na Sheria na stadi ya udereva wa Viongozi. Aidha, Wafanyakazi saba (7) wanaendelea na masomo, kati ya hao wanawake wawili (2) katika ngazi ya Stashahada ya Uzamivu, mwanamme mmoja (1) Shahada ya Pili, wafanyakazi wanawake wawili (2) Shahada ya Kwanza, mwanamme mmoja (1) Stashahada na mwanamke mmoja (1) Stashahada ya Cheti.

ii. Wafanyakazi 46 wamepatiwa likizo zikiwemo likizo ya kawaida kwa Wafanyakazi 28 (wanawake 16 na wanaume 12), likizo ya dharura wafanyakazi 14 (wanawake 9 na wanaume 5) na Wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa likizo ya uzazi. Aidha, jumla ya Wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa malipo ya mchango wa ufiwa na Wafanyakazi wanne (4) wamelipwa posho la Kukaimu pamoja na kulipa mishahara na stahiki zake kwa Wafanyakazi kupitia mfumo wa "Payroll System" kwa kuzingatia muundo wa malipo ya Serikali (Government Scheme of Service);

iii. Wizara ilifanya ununuzi wa Vifaa vya Ofisi na Usafiri ikiwemo mafuta, Kompyuta, vifaa vya kuandikia pamoja na viburudishaji. Manunuzi yamefanywa kwa kuzingatia mahitaji ya kazi, ubora na ufanisi, bei ya Ushindani na matakwa ya kizabuni kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

iv. Jumla ya Mikutano 19 ya majadiliano ya masuala ya Viwanda na Biashara imeratibiwa na kuhudhuriwa. Kati ya hiyo Mikutano sita (6) ya Kimataifa, Mikutano minne (4) Kikanda na Mikutano tisa (9) ya Kitaifa. Mikutano hiyo imejumuisha kikao cha 14 cha Kamati ya pamoja ya SJMT na SMZ, Kongamano la 19 la kukuza ushirikiano wa kibiashara kati ya India na Afrika na Kikao cha Enterprising Africa Traditional Network nchini Afrika Kusini; na

v. Katika kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi, Wizara imesimamia utoaji wa huduma mbali mbali zikiwemo kufanya malipo ya huduma ya usafi, kodi ya jengo, huduma ya umeme, huduma ya maji, gharama za mtandao na matengenezo madogo ya Ofisi.

31. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Ofisi ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.23** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi, 2025 Programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 1.71.** Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi bilioni 1.63** sawa na asilimia 95.0 zimeingizwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

**SR010102: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara**

32. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kutoa huduma za uandaaji na uibuaji wa tafiti, uandaaji na utekelezaji wa Mipango pamoja na usimamizi wa takwimu za Wizara. Utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imekamilisha Sera ya Biashara ya Mwaka 2024 pamoja na Ripoti ya Tathmini ya Mazingira ya Biashara ya mwaka 2025 ambapo Sera na Ripoti hizi zinalenga kutatua vikwazo katika ufanyaji Biashara na Uwekezaji nchini;

ii. Tathmini ya Kisheria na Kitaasisi ya kuimarisha Mazingira ya Biashara pamoja na Mpango wa Utekelezaji imekamilika ambayo inalenga kupunguza changamoto za wafanyabiashara pamoja na kurahisisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini;

iii. Taarifa ya takwimu za Biashara na Viwanda kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 zimekusanywa na kuandaliwa;

iv. Wizara imeandaa taarifa za takwimu za robo na nusu mwaka zinazohusiana na Biashara na Viwanda na kuziwasilisha Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali;

v. Wizara imeratibu uandaaji wa Rasimu ya Sera ya Miliki Bunifu (Intellectual Property Policy, 2024) na kwa sasa imewasilishwa Serikalini kwa ajili ya kupitiwa na kuridhiwa kwa matumizi;

vi. Wizara imefanya mapitio ya Mpango wa ufuatiliaji na Tathmini na Mkakati wa Mawasiliano ya Sera ya Biashara ya mwaka 2024 kwa kuiwasilisha kwa wadau na kufanikiwa kuiboresha mipango hiyo;

vii. Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta Binafsi imeandaa Rasimu ya Sheria ya Maendeleo ya Sekta Binafsi kwa lengo la kuimarisha na kuiwezesha Sekta binafsi kuwa muhimili wa ukuaji wa uchumi nchini;

viii. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa Julai hadi Machi, 2025 imeandaliwa; na

ix. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Tanzania Bara imeandaa pendekezo la mradi wa Mnyororo wa thamani wa mazao ya Mwani na Dagaa kwa Awamu ya III na kuwasilishwa Shirika la Biashara Duniani kupitia mfuko wa "Enhanced Integrated Framework (EIF)" pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa.

**33. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi milioni 522.76 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi, 2025 Programu ndogo hii ilipangiwa Shilingi milioni 414.70 na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi milioni 254.65 sawa na asilimia 61.4 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii na mishahara.

## SR010103: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

**34. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

**35. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

i. Jumla ya Viwanda 28 vimetembelewa vikiwemo viwanda tisa (9) vya mafuta ya mimea, viwili (2) vya maji ya kunywa, vitatu (3) vya mafuta ya Chikichi na nazi, kiwanda kimoja (1) cha chumvi cha Swahili Salt Coast, kiwanda cha Maseredani Chanjaani, Kiwanda cha Matenki ya Maji, viwanda vitatu (3) vya kusarifu na kukoboa nafaka, viwanda viwili (2) vya wazalishaji wa bidhaa za spice na kiwanda kimoja (1) Kiwanda cha Uzalishaji wa unga wa ngano ambacho kinatarajia kuanza uzalishaji karibuni na viwanda vidogo saba (7) vya Wajasiriamali wadogo . Aidha, jumla ya ajira 150 zimepatikana kwa vijana katika viwanda hivyo na kupunguza wimbi la vijana kuzurura mitaani;

ii. Vikao vitatu (3) vya kujenga uelewa wa Kanuni na Sheria ya Biashara vimefanyika ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwenye biashara kwa wafanyabiashara pamoja na kufanyika kwa vikao viwili (2) kwa lengo la kuzuia ongezeko la bei za bidhaa hizo muhimu za Mchele, Sukari na Unga wa Ngano na kupata nafasi ya kusikiliza Changamoto za wafanyabiashara hao na kuzitafutia ufumbuzi;

iii. Ziara katika maeneo ya maduka zimefanyika kwa maduka 972 ili kuhakikisha taratibu za biashara zinafuatwa ipaswavyo ikiwemo kufuata utaratibu wa kutumia bei elekezi katika ufanyaji wa biashara;

iv. Jumla ya vikundi 46 vya Wajasiriamali vimetembelewa na kufanyika kwa mikutano mitatu (3) kwa lengo la kusikiliza changamoto zao na kuweza kuzitatua katika Wilaya zote za Pemba. Aidha, jumla ya vikundi 13 vilishiriki katika Maonesho ya Saba Saba Tanzania Bara, vikundi 36 vimeshiriki siku ya Chakula na Maonesho ya Marashi ya karafuu pamoja na kuratibu ushiriki wa Maonesho yaliofanyika Sudan Novemba, 2024 kwa vikundi saba (7) vya Wajasiriamali wa Mwani na Mjasiriamali mmoja (1) kushiriki katika maonesho ya Biashara yaliyofanyika China Mwezi wa Septemba, 2024;

v. Wizara iliandaa Tamasha la Biashara Pemba ambalo lilikwenda sambamba na Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambapo jumla ya Taasisi za Serikali 44, Taasisi za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tano (5), Wafanyabiashara na Wajasiriamali 65 walishiriki katika Tamasha hilo pamoja na Viwanda Vitatu (3); na

vi. Jumla ya Wafanyakazi watatu (3) wakiwemo mwanawake mmoja (1) na wanaume wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani na

nje ya nchi katika fani za Utawala, Takwimu na Viwanda na Wafanyakazi watatu (3) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Biashara. Aidha, Wafanyakazi tisa (9) wamepatiwa likizo la kawaida, kati ya hao Wafanyakazi watano (5) wamepatiwa stahiki zao. Vile vile, vikao vinne (4) kwa Watendaji vimefanyika vilivyolenga kujenga uelewa wa Maadili ya Watumishi pamoja na masuala ya Mtambuka yakiwemo usawa wa jinsia pamoja na kujiepusha na rushwa.

36. **Mheshimiwa Spika,** Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 1.10** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025 programu hii ilipangiwa **Shilingi milioni 855.97.** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi milioni 621.21** sawa na asilimia 72.6 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**PR0102: Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji wa Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Programu hii ina jukumu la kuongeza mchango wa sekta ya uzalishaji Viwandani katika Pato la Taifa. Utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:-

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 40.75 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi, 2025, Programu hii ilipangiwa Shilingi bilioni 40.65 na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi bilioni 11.24 zimeingizwa sawa na asilimia 27.7 kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010201: Programu Ndogo ya Ukuzaji wa Viwanda**

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kutoa huduma za kuimarisha Sekta ya Viwanda. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

i. Wizara imeshiriki katika mikutano ya kupitia Kanuni za Mitaa ya Viwanda kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC-SEZ Regulation) iliyofanyika Jijini Dar es Salaam na Arusha pamoja na kushiriki vikao vinavyohusiana na uzalishaji wa Viwandani;

ii. Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Zanzibar iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali wanane (8) wenye Viwanda kutoka Zanzibar katika maonesho ya Viwanda yaliyofanyika Dar-es salaam;

iii. Wizara imekamilisha Mfumo wa Taarifa za Viwanda (Industrial Information System) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa ajili ya kupokea taarifa za viwanda ikiwemo

uzalishaji, ajira pamoja na changamoto mbali mbali za wenye viwanda na tayari umeshaanza kutumika rasmi; na

iv. Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda ya mwaka 2019 -2029 kwa lengo la kuifanya Sera hiyo iendane na mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisera na kisheria kutokea ndani ya Nchi na katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika Ukanda wa soko Huria la Afrika.

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 40.72** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025 programu hii ilipangiwa **Shilingi billioni 40.63** na hadi kufikia Machi 2025 jumla ya **Shilingi bilioni 11.24** sawa na asilimia 27.7 ya fedha zilizopangwa. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 11.17 ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo na Shilingi milioni 69.43 kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara.

**SR010202: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali**

41. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Maendeleo ya Wajasiriamali inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera ya Wajasiriamali na uendelezaji wa wajasiriamali na kuongeza mchango wa wajasiriamali wadogo na wa kati katika pato la

Taifa. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

i. Wizara, imeandaa Rasimu ya Utekelezaji wa Sera ya Ujasiriamali ya 2020. Utekelezaji wake utahusisha Taasisi na Wadau wakiwemo Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar, Idara ya Ushirika, Idara ya Maendeleo ya Vijana, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali na Jumuiya ya Taifa ya Wafanyabiashara Zanzibar;

ii. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan, inaendelea kutoa mafunzo ya Falsafa ya Kaizen. Falsafa hii imejikita katika kutoa elimu ya kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji Viwandani. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya kampuni saba (7) zimeshiriki ikiwemo kampuni ya 'Lootah Group' , Inaya Zanzibar, 'Metal Man Company', 'Safari Water Company Ltd', 'Zanzibar Sugar Factory Ltd', 'Zanpackaging Group' na 'Aishan Pvt. Ltd'. Aidha, washiriki 14 kutoka Sekta ya Umma na Binafsi wamenufaika na kupata vyeti vya kuwa wakufunzi wa falsafa ya Kaizen nchini. Aidha, Kampuni ya INAYA Zanzibar imeshinda tunzo ya mwaka ya kitaifa ya KAIZEN (Tanzania KAIZEN Award 2025), yaliyofanyika Jijini Dar-Es-Salaam Machi 13, 2025 ambapo

kampuni hiyo imeteuliwa kushiriki shindano la mwaka la Afrika Kaizen nchini Afrika ya kusini (The Africa Kaizen Award 2025, South Africa).

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 33.55** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi, 2025. Programu hii ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 22.42** na hadi kufikia Machi 2025, program hii ndogo haikuingiziwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Hii imetokana na fedha zaprogramu hii zilikuwa zikitumika na Taasisi ya SMIDA ambaye majukumu yake yamehamishiwa Wakala wa Uweshaji wananchi Kiuchumi, Zanzibar.

## PR0103: Programu Kuu ya Ukuzaji Na Uendelezaji wa Biashara

43. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inasimamiwa na Idara ya Biashara pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Programu hii ina Programu ndogo tatu ambazo ni :-

i. Programu ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji.

ii. Programu ya Uwezeshaji Biashara.

iii. Programu ya Utengamano wa Kibiashara.

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kuu ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 15.65 kwa mwaka wa fedha

2024/2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi, 2025, Programu hii ilipangiwa Shilingi bilioni 14.39 na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi bilioni 4.65 zimeingizwa sawa na asilimia 32.4 kwa ajili ya kutekeleza programu hii. Utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika kila programu ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo: -

**SR010301: Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji**

**45. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imeratibu na kuandaa Tamasha la kumi na moja (11) la Biashara la mwaka 2025, ambalo hufanyika kila ifikapo Januari ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025 jumla ya washiriki 338, kati ya hao Taasisi za Serikali 85, Kampuni 20, Vyama vya Ushirika 10, Wafanyabiashara na Wajasiriamali 223 walishiriki katika Tamasha hilo. Aidha, Wafanyabiashara wadogo 11 kutoka nje ya nchi walishiriki, kati ya hao, watano (5) kutoka Uganda, wawili (2) Burundi na nchi za Kenya, Misri, India na Zambia zimekuwa na ushiriki wa moja kwa moja;

ii. Wizara imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) ambapo jumla ya washiriki 52 kutoka

Zanzibar walishiriki. Kati ya hao, Wajasiriamali 41, Taasisi za Serikali tisa (9) na Kampuni Binafsi mbili (2) zimeshiriki;

iii. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji imeratibu ushiriki wa Wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonesho ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaliyofanyika tarehe 26 Oktoba hadi tarehe 5 Novemba 2024 nchini Sudani ya Kusini ambapo jumla ya Wajasiriamali 45 (wanaume 10 na 35 wanawake) wameshiriki.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 10.36** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 10.24** hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi bilioni 1.84** sawa na asilimia 18.0 ziliingizwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 1.70** ziliingizwa kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **Shilingi 131.94** zimeingizwa kwa ajili ya kazi za kawaida na mishahara.

**SR010305: Programu Ndogo ya Uwezeshaji Biashara**

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Biashara pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ambazo zina jukumu la kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

i. Kufanyika kwa ukaguzi katika maeneo ya uingizaji na usafirishaji bidhaa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi kwa Wafanyabiashara ambapo kupitia ukaguzi huo, Wafanyabiashara 166 wamepatiwa hati za usajili wa biashara (Import /Export Registration Certificate);

ii. Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imefanya mafunzo ya Urasimishaji wa Biashara kwa wafanyabiashara 770 kwa Unguja na Pemba ambapo kati ya hao wafanyabiashara 250 katika Wilaya ya Mjini Unguja, 200 Wilaya ya Kaskazini A Unguja, 200 Wilaya ya Wete Pemba, 70 Wilaya ya Kusini, na 50 Wilaya ya Magharibi B kwa lengo la kuwahamasisha wafanyabiashara kufanya biashara kwa kutumia mifumo iliyo rasmi;

iii. Uchambuzi wa Mapitio ya Kanuni za Mamlaka zinazosimamia Leseni, Vibali, Ada, Tozo na Ruhusa nyengine za ufanyaji biashara kwa sekta kumi (10) umefanyika;

iv. Muongozo wa utoaji leseni na vibali kwa Mamlaka za utoaji leseni umeandaliwa ambapo umejumuisha misingi, vigezo, taratibu, hatua na muda wa upatikanaji leseni;

v. Wizara imesimamia Mamlaka za utoaji leseni 57 kutumia mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma ambapo maombi ya leseni na vibali yamefanyika kupitia mifumo ya kielektroniki

sambamba na Malipo ya leseni na vibali kulipwa kupitia Benki;

vi. Utafiti mdogo kuhusu ufuatiliaji wa mwenendo wa biashara kisiwani Pemba umefanyika na kuweza kugundua changamoto mbalimbali zikiwemo utitiri wa Taasisi katika ukusanyaji tozo. Aidha, Wizara imezitolea miongozo na kuziwasilisha kwa Mamlaka husika ili kupatiwa ufumbuzi wa haraka;

vii. Jumla ya Mamlaka 22 za utoaji leseni Unguja na Pemba zimefanyiwa ukaguzi na kupatiwa maelekezo ya kuandaa Kanuni na majadweli ya tozo kwa Mamlaka ambazo hazina kanuni au kanuni zao zimepitwa na wakati;

viii. Ripoti ya awali ya Utafiti wa Mazingira Wezeshi ya Ufanyaji Biashara 2023-2025 (Zanzibar Business Enabling Environment) imeshatayarishwa;

ix. Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi na Utoaji Leseni imefanya Uchambuzi wa Mapitio ya Kanuni za Mamlaka zinazosimamia Leseni, Vibali, Ada, Tozo na Ruhusa nyengine za ufanyaji biashara kwa sekta kumi (10) ambazo ni Uwekezaji kanuni nne (4), Utalii kanuni kumi (10), Biashara kanuni sita (6), Sekta ya Afya kanuni tatu(3), Sekta ya Elimu kanuni moja(1), Sekta ya Nishati kanuni mbili (2), Sekta ya Kilimo kanuni moja(1), , Sekta ya Maliasili na Misitu kanuni moja(1), Sekta ya

Mifugo kanuni moja(1) na Sekta ya Uchumi wa Buluu kanuni moja (1);

x. Wizara imefanikiwa kusimamia Mamlaka za Utoaji Leseni kutumia mifumo ya kielektroniki katika kutoa huduma ambapo maombi ya leseni na vibali yatafanyika kupitia mifumo ya kielektroniki sambamba na Malipo ya leseni na vibali kulipwa kupitia Benki;

xi. Mkutano wa sita (6) wa Baraza la Taifa la Biashara umefanyika pamoja na vikao viwili (2) vya Kamati Tendaji ya Baraza vimefanyika kwa ajili ya kupitia utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa katika Jukwaa la 12 la Biashara. Aidha, Jukwaa la 13 la Biashara limefanyika na washiriki 350 wameweza kuhudhuria kutoka Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Mabalozi na Watendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

xii. Wizara imekutana na Wawekezaji na Wafanyabiashara wakubwa kwa ajili ya kuwapa elimu juu ya uwepo wa Baraza la Ushindani Halali wa Biashara na majukumu yake. Miongoni mwa Wawekezaji hao ni Azam Marine Company Limited, Davis & Shirtliff (Zanzibar) Limited, Al-Hilal General Trading Co. Ltd, CPS Sales Limited, Tanzania Cigarate Company, Estim Enterprises Ltd, Derm Elevator Ltd, ASB Holdings Catering Service Ltd, Fundu Lagoon, MB Home, ABSA

bank, AMANA bank ambapo wameahidi kulitumia Baraza endapo watakwazwa katika biashara zao;

xiii. Wizara imewajengea uwelewa pamoja na kuzisajili Taasisi za Mamlaka za Udhibiti kuhusiana na matumizi ya mfumo wa uendeshaji wa mashauri ya rufaa;

xiv. Uhakiki kwa mita za vituo vya mafuta 654, mita 45 za bohari na uwanja wa ndege, mizani 601, gari za kusambazia mafuta 23 na Matangi 69 ya mafuta umefanyika. Aidha jumla ya viwanda sita (6) vinavyozalisha unga wa ngano, sukari, tomato maji na gesi vimehakikiwa;

xv. Wizara imefanya uhakiki wa ujazo wa mafuta ya Meli Unguja na Pemba katika mfumo wa pamoja kwa lita 194,142,308 pamoja na kupokea meli saba (7) ambazo zilishusha kilo 6,507,004 za gesi;

xvi. Wizara imefanya uchunguzi maalum wa bidhaa ya Sukari kwa baadhi ya waingizaji (Importers) na Sub dealers katika soko la Zanzibar kwa lengo la kubaini iwapo wafanyabiashara hao wanatekeleza mienendo ya biashara inayokatazwa na imebainika kuwa baadhi ya wafanyabiashara hawana uelewa wa elimu ya ushindani. Hivyo, Wizara imewapatia elimu ya mienendo ya biashara inayokatazwa Sokoni kwa mujibu wa Sheria nambari 5 ya mwaka 2018;

xvii. Wizara imefanya ukaguzi wa maduka 647, maghala 91 na Supermarket 38. Ukaguzi huo ulilenga bidhaa za vyakula vya makopo na bidhaa za matumizi ya binaadamu pamoja na kufanya ukaguzi kwa bidhaa zilizodhibitiwa kama vile sukari, mchele wa mapembe na unga wa ngano. Katika ukaguzi huo ilibainika kwamba wafanyabiashara wawili (2) walipatikana na kosa la kuuza mchele vipolo 330 vya kilo 50 wenye thamani ya Shilingi 21,450,000 ambao sio salama kwa matumizi ya binaadamu. Wafanyabiashara hao walitozwa faini na kulipa gharama ya utekelezaji. Wizara pia iliwapa uelewa wa Sheria Namba 5 ya Mwaka 2018 na kutakiwa kufuata taratibu za ufanyaji biashara kwa uhalali;

xviii. Wizara inaendelea kusimamia bei elekezi ya bidhaa zinazodhibitiwa zilizopangwa na Serikali kwa bidhaa za sukari, mchele wa Mapembe, unga wa ngano, mafuta ya kula na saruji;

xix. Wizara imebaini uwepo wa Miungano ya Makampuni baina Kampuni ya MSG Hotel Resort Limited na Magdy Samir Nagub kununua asilimia 100 ya hisa za Kampuni ya Girogest Limited, Kampuni ya Reliance Resort & Spa limited kununua hisa za Kampuni ya Uroa bay, Kampuni ya Reliance Resort & Spa limited kununua hisa za Kampuni ya Samaki Beach Lodge, Kampuni ya Daria Holdings Limited kununua asilimia 80 ya hisa za Kampuni ya Fumba Port Limited wamepatiwa elimu ili

kufuata utaratibu wa kisheria wa kuwasilisha taarifa zao kwa lengo la kuidhinishwa na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara;

xx. Wizara imefanya ukaguzi wa maeneo 284 ya watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara ikiwemo Hoteli 137, Kumbi za burudani tatu (3), Vyuo vikuu vitatu (3), Vituo vya Utangazaji viwili (2), Maduka 142 ya kuuza na kudodisha Vinasa Sauti na Picha kwa lengo kuangalia uhalali wa matumizi ya leseni zao;

xxi. Leseni 88 kwa Watumiaji halali wa kazi ya hakimiliki zimetolewa kwa Unguja na Pemba zikiwemo 50 za Hoteli, mbili (2) za Vituo Vya Utangazaji, tatu (3) Kumbi za Burudani na 33 Maduka ya kukodisha Vinasa sauti na picha. Aidha, hafla ya mgao wa 11 wa Mirabaha umefanyika ambapo wafanyabiashara ya hakimiliki 1,338 wamefaidika na kiasi cha Shilingi Milioni 157 zimetumika katika mgao huo;

xxii. Malalamiko manne (4) ya uvunjwaji wa hakimiliki yamepokelewa na kusikilizwa na Wizara kuyatolea maamuzi ikiwemo kulipa fidia kwa hasara iliyopatikana. Malalamiko mawili (2) yanahusiana na matumizi ya picha katika kitabu bila ya ridhaa ya mwenye picha, matumizi ya nyimbo bila ya ridhaa ya mmiliki wa nyimbo na matumizi ya picha ya msanii katika tangazo la Tamasha la ndani ya Hoteli bila ya ridhaa ya msanii husika;

xxiii. Wizara imeandaa na kurusha hewani vipindi 11 kupitia Televisheni na Redio.Makala moja (1) na Vipeperushi juu ya masuala ya hakimiliki vimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau kupitia kurasa za mitandao ya kijamii ya COSOZA. Aidha, wadau 147 wamepatiwa elimu juu ya masuala ya hakimiliki katika Maonesho ya kimataifa ya Biashara ya mwaka 2025;

xxiv. Wizara imefanya Mapitio ya Sheria ya Hakimiliki (Namba 14) ya mwaka 2003 kwa lengo la kuimarisha Usimamizi na Ulinzi wa Hakimiliki; na

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 5.24** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2024 – Machi 2025 programu ndogo hii ilipangiwa **Shilingi bilioni 4.11** na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi Bilioni 2.80** sawa na asilimia 68.2 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

**SR010306: Programu Ndogo ya Utengamano wa Kibiashara**

**49.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha biashara huria ambayo itapelekea kuongezeka kwa masoko na uwekezaji baina ya Zanzibar na Nchi nyengine. Utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika hatua ya kuimarisha Mashirikiano ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa imeweza kushiriki katika mikutano mbali mbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na masuala ya Biashara. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya uwezeshaji biashara ikiwa na lengo la kurahisisha ufanyaji wa biashara nchini, Mkutano wa Baraza la Kisekta la Biashara, Uwekezaji na Fedha la Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye lengo la kuweka taratibu sawa za ufanyaji biashara, uwekezaji na masuala yote yanayohusiana na fedha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkutano wa uondowaji wa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha na Mkutano wa biashara ya huduma;

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki katika vikao vya uanzishwaji wa mfumo wa pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshaji Shehena maeneo ya forodha kwa ngazi ya Wataalamu na Makatibu Wakuu. Mfumo huo wa kielektroniki una lengo la kurahisisha uondoshaji na usafirishaji wa shehena Nchini. Aidha, katika kuimarisha uhusiano wa kibiashara na Tanzania Bara ni pamoja na kikao cha uandaaji wa Sheria ya Ahueni za Biashara (Trade Remedy Act), Kikao cha kupitia ***Taariff offer*** ya bidhaa zilizopo katika kundi B na C kwa ajili ya ufunguaji wa Soko Huru la Afrika na kikao cha kujadili ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na Korea ikiwa na lengo la kufanya uchambuzi wa maeneo ya kiuchumi

ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kushirikiana na Jamhuri ya Korea.

## 8.0 MASHIRIKIANO NA MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA (TANTRADE)

52. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Biashara na Viwanda na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya nje kwa bidhaa zinazozalishwa ndani ya Zanzibar, hufanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania ili kuhakikisha biashara inakuwa nchini.Miongoni mwa maswala makuu ambayo Wizara imeshirikiana na TANTRADE kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025 ni pamoja na:-

i. Mashirikiano katika Uratibu wa maonesho mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yakiwemo Maonesho ya 48 ya Biashara ya Sabasaba ambapo kwa upande wa Zanzibar Taasisi mbalimbali za binafsi na Serikali pamoja na Wajasiriamali walishiriki katika maonesho hayo; Maonesho ya Viwanda, Maonesho ya 11 ya Kimataifa ya Biashara ya maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika Dimani.

ii. Wizara inashirikiana na TANTRADE katika kuhakikisha kuwa taarifa na taratibu za usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa nchini zinapatikana kwa urahisi kwa kupitia mfumo wa Trade Portal.

Baadhi ya taarifa za bidhaa zinazoingizwa na kusafirishwa tayari zimeshaingizwa katika mfumo huo zikiwemo bidhaa za mchele, sukari, karafuu, mwani, dawa, bidhaa za viungo, asali, na bidhaa nyengine. Taarifa zilizoingizwa kwenye mfumo huo zinaonesha taratibu za kufuata na vibali vinavyohitajika wakati wa uagizaji na usafirishaji bidhaa nchini.

53. **Mheshimiwa Spika,** Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi milioni 43.84 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2024 – Machi 2025 programu ndogo hii ilipangiwa Shilingi milioni 32.52 na hadi kufikia Machi 2025, programu ndogo hii imeingiziwa Shilingi milioni 9.02 kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

## 9.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024-MACHI 2025.

54. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipanga kutumia Shilingi Bilioni 50.32 kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili (2) ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi bilioni 40.32 kwa ajili ya mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Park) na Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya mradi wa kuendeleza Uwanja wa Maonesho ya Kimataifa Dimani. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

### 9.0.1 Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda

55. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuanzisha maeneo Tengefu ya Viwanda kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kutengeneza bidhaa za Viwandani, kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuongeza mauzo ya nje. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mradi huu ulipangiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 40.32.** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, mradi ulipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 40.32** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 11.17** zimeingiziwa sawa na asilimia 27.7 ya makadirio kwa mwaka. Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo: -

i. Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda inaendelea kuimarisha eneo la Mtaa wa Viwanda liliopo Dunga Zuze na hadi nawasilisha makadirio ya bajeti ya Wizara hii zkwa mwaka 2025/2026 ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 7.83 umefikia asilimia 95 na kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika kwa asilimia mia moja 100.

ii. Wizara imempata Mshauri Elekezi kutoka Kampuni ya AE & Q Consult Limited kwa ajili ya uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan), kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira na Jamii (Environmental and Social Impact Assessment) na Uchunguzi wa Udongo

(Geo Technical Investigation) katika Mtaa wa Viwanda Pangatupu.

iii. Kupatikana Mshauri Elekezi kampuni ya NIMETA Consult (T) Ltd kwa ajili ya kuandaa michoro ya ukuta wa uzio (Fence Wall), jengo la utawala na majengo ya Viwanda (fabricated steel structure Industrial Sheds) kwa Mtaa wa Viwanda Dunga Zuze. Aidha, kwa upande wa Chamanangwe ubunifu wa michoro ya ukuta wa uzio (Fence Wall), jengo la utawala na majengo ya Viwanda (fabricated steel structure Industrial Sheds), ubunifu wa michoro ya Barabara (Internal Roads) na Miundombinu ya maji (Water Tank, Pipe Distribution and Borehole) imefanyika. Kwasasa Mshauri Elekezi ameshakamilisha kazi zote za ubunifu na uandaaji wa nyaraka hizo na tayari Wakandarasi wa ujenzi wa miradi hiyo wameshapatikana.

iv. Kupatikana Mkandarasi Kampuni ya Simba Developer Ltd, kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya maji (Water Tank, Pipe Distribution and Digging of Borehole) katika Mtaa wa Viwanda Chamanangwe.

v. Kupatikana Mkandarasi kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa ajili ya ujenzi wa ukuta wa uzio (Fence Wall) na majengo ya Viwanda (Industrial Sheds) kwa Mtaa wa Viwanda Chamanangwe na Dunga na

ujenzi wa Barabara za ndani (Internal Roads) katika Mtaa wa Viwanda Chamanangwe.

### 9.0.2 Mradi wa Kuyaendeleza Maeneo ya Maonesho ya Biashara Dimani.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa kuliendeleza eneo la kisasa kwa ajili ya maonesho ya Kimataifa Zanzibar. Eneo tayari linatumika kwa shughuli mbalimbali ikiwemo maonesho ya ndani na ya Kimataifa na mikutano mbalimbali. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni 10** na hadi kufikia Machi, 2025 mradi huu umeingiziwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1.70** sawa na asilimia 17.1 ya fedha hizo. Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara imefanya malipo kwa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ikiwa ni malipo ya kazi zilizofanyika katika kituo cha maonesho Dimani zikiwemo ujenzi wa mindombinu ya vyoo, uwekaji wa vizege katika njia za watembea kwa miguu kuelekea katika mashamiana, kujenga minara na kuweka matangi manne (4) ya kuhifadhia maji, kujenga vibaraza vya kuweka mashamiana makubwa 10 yenye ukubwa wa mita 50 kwa 20 na madogo kumi (10) yenye ukubwa wa mita 6 kwa 6; kujenga vibaraza vya ukumbi wa mikutano wenye ukubwa wa mita 50 kwa 50; kujenga vibaraza vya

shamiana la chakula; kujenga ukuta; kujenga vibanda vya walinzi; vibanda vya kununulia tiketi; vibaraza vya shamiana la VIP lenye ukubwa wa mita 12 kwa 10 pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la utawala kwa hatua ya msingi;

ii. Wizara imefanya kazi ya uimarishaji wa ukumbi wa mikutano wa Dk Hussen Ali Mwinyi kwa kuweka madirisha ya vioo.

iii. Wizara imejenga vyoo vya watu mashuhuri na kibanda cha kuhifadhia umeme ambapo ujenzi wake unaendelea.

### 9.0.3 Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar.

**57. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZBS imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa kuendelea na ununuzi wa vifaa vya maabara pamoja na ujenzi wa Maabara. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 ZBS imeweza kutekeleza miradi minne (4) kama ifuatavyo:-

**58. Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Maabara ya Metrolojia umeweza kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Ujenzi wa maabara ya Metroloji umekamilika kwa asilimia 100

ii. Zabuni ya ununuzi wa vifaa vya “Temperature na Mass” imeshafanyika na Mzabuni

ameshawasilisha vifaa vitano (5) kati ya sita (6) alivyotakiwa kuwasilisha ambavyo ni *(High performance precision, balance, Set weight – class F, Dehumidifier, Digital barometer, na Set weight –class E)* na kifaa kimoja (1) ambacho hakijawasilishwa ni *(Laboratory granite ant-vibration table)".*

**59. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ununuzi wa Mtambo wa Kupima Mita za Umeme Mzabuni yupo katika hatua ya kuwasilisha Mtambo huo katika Taasisi lakini amepata changamoto ya kukwama kwa kontena iliyopakiwa mtambo huo katika bandari ya Singapore na Mombasa. Aidha, Mzabuni ameomba muda wa nyongeza kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo ambapo Mzabuni ametakiwa kukamilisha kazi mnamo tarehe 23/05/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ununuzi wa vifaa vya Maabara ya Petroleum umetekelezwa ambapo Mzabuni amewasilisha vifaa viwili (2) ambavyo ni *((Density meter na Smoke point tester).*

**60. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025 miradi hii ilipangiwa jumla ya Shilingi 2,100,747,464.00 Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi 2,014, 736,928.86 Zimetumika sawa na asilimia 95.9

## 10.0 MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE 2021/2022 - 2024/2025

**61. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Uongozi wa Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Wizara imefanikiwa kutekeleza mambo makuu yafuatayo:

### 10.0.1 Kuimarisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda

**62. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo katika kuimarisha sekta ya viwanda nchini.

i. Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Nchi (GDP) kutoka asilimia 19.6 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia asilimia 20.8 kwa mwaka 2023/2024 ambayo imechangiwa na kuimarika kwa uzalishaji viwandani, Serikali kuekeza katika miradi mikubwa na kuanzishwa kwa viwanda vipya;

ii. Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda inaendelea kuimarisha eneo la Mtaa wa Viwanda liliopo Dunga Zuze , ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 7.83 umefikia asilimia 95 na kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya maji umekamilika kwa asilimia mia moja 100;

iii. Wizara imepokea maombi saba (7) ya Wawekezaji wa miradi ya Viwanda kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili wa uwekezaji wa eneo la Viwanda Dunga. Aidha, Wizara imetoa hati kwa Taasisi ya

Viwango Zanzibar ZBS kwaajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha huduma za maabara za upimaji wa bidhaa za aina zote zitazozalishwa ndani na nje ya Zanzibar (ZBS Centralized Laboratories). **Angalia Kiambatanisho Nambari 5**

iv. Wizara kwa kushirikiana na Serikali Mtandao imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Takwimu za Viwanda (Industrial Information System) na sasa umeshaanza kutumika kwa ajili ya kukusanya taarifa muhimu za viwanda kwa wakati (real time) ambazo zitaisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi ya kisera na ya kimkakati katika kutatua changamoto zinazozorotesha ukuaji wa viwanda vya ndani hapa nchini;

v. Kuwepo kwa Mpango wa Matumizi ya ardhi kwa maeneo ya viwanda Dunga Zuze na Chamanangwe;

vi. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani kilichopo Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba ambacho kimelenga kuleta mapinduzi ya soko la mwani kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na kinatarajiwa kuchakata mwani tani 30,000 kwa mwaka;

vii. Kuongezeka kwa bei ya Mwani kutoka Shilingi 600 kwa kilo moja kwa mwaka 2020 mpaka Shilingi 1,000 kwa Mwani aina ya Spinosum kwa mwaka 2024 na Shilingi 1,000 kwa kilo moja kwa mwaka 2020 mpaka Shilingi 2,100 kwa Mwani aina ya Cottonii kwa mwaka 2024. Pia Wizara imeweza

kununua mwani aina ya Ulva ambao kwa shilingi 800 kwa kilo kutoka kwa wananchi; na

viii. Wizara imefanikiwa kugawa vifaa vya kulimia Mwani vikiwemo boti na mashine ambapo vikundi 204 vimepatiwa boti na mashine na vikundi 304 vimepatiwa vifaa vya kulimia mwani.

### 10.0.2 Kuimarika kwa Sekta ya Biashara

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini kwa kuimarisha fursa za masoko na uwezeshaji biashara kama ifuatavyo:-

**1. Fursa za masoko**

i. Wizara imefanikiwa kujenga eneo la Maonesho ya Biashara huko Dimani, eneo lina ukubwa wa ekari 11 ambapo limejumuisha ukumbi mkubwa wa mikutano ( mita 50 kwa 50) wenye uwezo wa kuchukua wastani wa zaidi ya watu 1,500, kumbi tisa (9) za maeonesho (mita 50 kwa 20) kwa kila moja ambazo zina uwezo wa kutoa kumbi ndogo ndogo 576 ( mita 3 kwa 3 ) kwa kila moja , vyoo 144, eneo la chakula lenye jumla ya vibanda 34, eneo la jengo la utawala, maeneo ya wafadhili na shamiana moja la Wageni mashuruhi. Wizara inaendelea kulitangaza eneo hili kwa Wawekezaji na Wafanyabaisha kuweza kutumika muda wote na kuongeza pato la nchi. Aidha, uwepo

wa Kituo hicho kumewasaidia wajasiriamali na wafanyabiashara kupata fursa ya masoko kwa kutangaza na kuuza bidhaa zao na huduma wanazozitoa, sambamba na kuitangaza Zanzibar kimataifa;

ii. Mpango wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) ya eneo la Kituo cha Kimataifa cha Biashara na Mikutano – MICE katika eneo la Dimani umeandaliwa. Kuwepo kwa Mpango huu kunatoa fursa kwa Wawekezaji kufanya maamuzi ya eneo la kuwekeza katika Kituo hicho;

iii. Wizara imefanikiwa kuratibu na kuandaa maonesho, ambapo jumla ya maonesho manne yalifanyika ikiwemo Tamasha la Biashara ambalo limefanyika kwa miaka mitatu (2021, 2022 na 2023) katika viwanja vya Maisara. Serikali imeandaa Maonesho mawili ya 10 na 11 ya Biashara yaliyofanyika Januari, 2024 na 2025 katika kituo kipya cha maonesho ya Biashara, Dimani. Maonesho hayo yalihudhuriwa na washiriki 714, kati ya hao washiriki 498 kutoka Zanzibar, 195 kutoka Tanzania Bara na 21 kutoka Nje ya Tanzania (Uganda, Burundi, Zambia, Misri, Kenya, Rwanda na India). Aidha, katika washiriki hao Taasisi za Serikali ni 219, kampuni kubwa ni 63 na wafanyabiashara wadogo, (wajasiriamali) ni 422 na Mashirika 10;

iv. Kuongezeka kwa bei ya kununulia Karafuu kutoka shilingi 14,000 kwa kilo kwa karafuu za daraja la I, Shilingi 13,000 kwa karafuu za daraja la II, na shilingi 12,000 kwa karafuu za daraja la III na mpeta umenunuliwa kwa shilingi 7,000 kwa kilo kwa mwaka 2021/2022. Aidha, Serikali imeweza kununua karafuu kutoka kwa mkulima kwa shilingi 15,000 kwa karafuu za daraja la I, shilingi 13,500 kwa karafuu za daraja la II, 12,500 kwa karafuu za daraja la III na mpeta kwa shilingi 7,000;

v. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025 Wizara imefanikiwa kununua kiasi cha tani za karafuu 16,614.48 kwa gharama ya shilingi 223.48 bilioni na kuuza nje ya nchi jumla ya Tani 16,214.11 kwa thamani ya shilingi 293.04 bilioni;

vi. Wizara imefanikiwa kuanza kutumia mifumo ya Ki-elektroniki katika kununua karafuu kwa wakulima na kuuza kwa kufanya mnada kupitia mifumo hiyo;

vii. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar Wizara imeweza kusafirisha karafuu kupitia bandari ya Mkoani Pemba kwenda moja kwa moja katika masoko ya nje;

viii. Wizara imeongeza vyungu viwili (2) vipya (Field Distillation Unit) ambavyo vimefungwa katika

Shamba la Mtakata kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mimea;

ix. Wizara imefanikiwa kuendelea na uzalishaji wa mafuta ya makonyo ya karafuu na mimea ikiwemo mkaratusi, mchaichai na mrehani. Uzalishaji huu unafanyika katika kiwanda cha makonyo Wawi Pemba na vyungu vya kusindika mafuta vilivyopo Pemba. Mapato yatokanayo na uzalishaji huu yameongezeka kutoka Shilingi 289 milioni kwa mwaka 2019/2020 hadi kufikia Shilingi 727 milioni mwaka 2023/2024; na

x. Wizara imekamilisha jengo la Kitega uchumi Madungu Chake Chake Pemba ambalo litaongezea Shirika Mapato mbali mbali na kutotegemea zao la karafuu pekee.

## 2. Uwezeshaji biashara.

i. Wizara imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa magari na pikipiki katika eneo lililopo mkabala na Ofisi za ZBS Maruhubi ambacho kina uwezo wa kukagua vyombo vya moto 300 kwa siku;

ii. Kuthibitishwa kwa ZBS na Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO) kupitia Mfumo wa Usimamizi Ubora (QMS) kwa kiwango cha ISO 9001:2015;

iii. Wizara imefanikiwa kuanza upimaji wa mafuta ya nishati yanayoingizwa nchini ambayo ni Petroli,

Diseli na mafuta ya ndege ambapo jumla ya lita zipatazo 631,614,486 zimeweza kupimwa;

iv. Wizara imefanikiwa kuzindua maabara ya vifungashio, nguo na ngozi, vimelea pamoja na uimarishaji wa maabara ya umeme kwa lengo la kupima ubora wa bidhaa ambazo zinazalishwa na zinaingizwa nchini;

v. Wizara imeweza kukusanya Mirabaha yenye thamani ya shilingi 693,063,962 kutoka kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara. Mirabaha hiyo imegaiwa kwa Wafanyabiashara 2,000 ambao wamesajili kazi zao;

vi. Wizara imeibadilisha dhana ya ubunifu kuwa ni dhana ya kibiashara kwa maslahi ya kiuchumi ya wabunifu na Taifa badala ya kuwa dhana ya kiutamaduni ambayo ilikuwa ikidhaniwa kuwa ni mali za jamii;

vii. Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imefanikiwa kuandaa majukwaa mawili (2) ya Biashara ambayo yalilenga kutatua changamoto za ufanyaji biashara Zanzibar;

viii. Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imeandaa Mkakati wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara unaojulikana kama (Blueprint for Regulatory Framework on the Improvement of Business Environment) ambao unalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji

nchini. Mkakati huu umefanya tathmini na mapitio ya Sera, sheria, kanuni, taasisi na miongozo inayohusiana na masuala ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji kwa ajili ya kuweza kuainisha mapungufu yanayokwamisha shughuli za biashara na uwekezaji. Hivyo, utekelezaji wa mapendekezo ya Mkakati huu unakusudia kuimarisha mazingira ya biashara nchini kwa kupunguza au kuondoa changamoto mbalimbali katika ufanyaji Biashara;

ix. Wizara imeweza kuimarisha huduma za usajili wa Biashara na Mali ndani ya masaa 24 kwa mteja ambae ombi lake limekamilika kwa kufuata masharti na vigezo vya usajili; na

x. Kuanzishwa Kwa Sheria ya Mmiliki Mnufaika ambapo sheria hiyo itasaidia kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili wa Mmiliki Mnufaika ambao utawezesha Serikali kuwafahamu Wamiliki Wanufaika wa Biashara zao.

## 11.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI AMBAZO HAZIPOKEI RUZUKU SERIKALINI ZINAZOSIMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 - MACHI 2025.

### 11.0.1 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

**64. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ZBS ilipangiwa jumla ya **Shilingi**

**6,342,025,280.20** kwa ajili ya kutekeleza kazi zake. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,055,709,289.36** kwa ajili ya kazi za kawaida na **Shilingi 2,100,747,464.00** Kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 ZBS imetumia jumla ya **Shilingi 6,070,446,217.22** sawa na asilimia **95.72** aidha, ZBS ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi 6,495,179,440** Kutokana na vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia Machi, 2025 imeweza kukusanya **Shilingi 6,973,323,280.11** Sawa na asilimia **107.36**

**65. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025 ZBS imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Leseni 15 za matumizi ya Alama ya Ubora kwa bidhaa zimetolewa kwa kutumia kiwango cha Zanzibar (ZBS Quality Mark). Aidha, vyeti 27 vimeuhuishwa baada ya kumaliza muda wake wa matumizi;

ii. Jumla ya shehena 876 za bidhaa nyenginezo zimekaguliwa kwa mfumo wa PVoC na kupewa vyeti vya ubora na Mawakala wa Ukaguzi nje ya nchi. Aidha, Kontena 6,315 za futi 40 na Kontena 5,562 za futi (20) zimekaguliwa kupitia Mfumo wa DI. Vile vile, jumla ya shehena 4,893 za bidhaa mbalimbali zimekaguliwa kupitia Uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar;

iii. Kwa upande wa vyombo vya moto vilivyotumika, jumla ya gari 3,976, pikipiki 4,641 zilizoingia nchini zimekaguliwa. Aidha, jumla ya lita 175, 512,956 za Mafuta ya Nishati zimekaguliwa kupitia Mfumo wa DI. Pia, kaguzi 45 za bidhaa katika maeneo ya sokoni zimefanyika.

iv. Jumla ya viwango 86 vimeandaliwa, kati ya hivyo viwango 25 vya bidhaa za chakula, 7 bidhaa za kemikali, 2 viwango vya kemikali viwandani na maabara, 6 mazingira, 10 bidhaa za umeme na elektroniki, 11 vifaa vya ujenzi, 6 nguo na ngozi, 4 viungo, 5 uhandisi mitambo na vyombo vya moto, 5 vya nyama, ndege, mayai, maziwa na bidhaa zinazohusiana na wanyama na ndege, 4 vya samaki na bidhaa za baharini na 1 huduma za utalii;

v. Jumla ya viwango 123 vimeweza kuuzwa kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025, kati ya hivyo viwango 38 vya bidhaa za kemikali, 69 bidhaa za chakula, 1 umeme, 3 uhandisi mitambo, 6 mazingira, 1 vifaa vya ujenzi na 5 viungo vya huduma;

vi. Sampuli 2,081 za bidhaa zimepokelewa, kati ya hizo sampuli 514 zilizofanyiwa uchunguzi wa kimaabara hazikukidhi matakwa ya viwango husika. Aidha, uwezo wa maabara umeongezeka ambapo ZBS kwa sasa ina maabara nane (8)

zinazofanya kazi ya uchunguzi katika mwaka 2024/2025;

vii. ZBS kupitia kiwango cha Kimataifa cha upimaji katika maabara **ISO/IEC 17025:2017** imefanikiwa kupata ithibati (Accreditation) katika maabara mbili (2) ya Mafuta ya nishati na Chakula Kemikali;

viii. ZBS imeshiriki majaribio ya (Proficiency Testing – PT) kwa maabara ya Umeme na Elektroniki imefanya PT – 2, Vifungashio PT – 1, Nguo na Ngozi PT – 1, Vimelea PT – 1, Petroleum PT - 1 na Maabara ya Chakula Kemikali imefanya PT- 3 kwa mujibu wa matakwa ya kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 katika taratibu za kupata ithibati ya maabara hizo;

ix. Watendaji 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na Watendaji 39 mafunzo ya muda mfupi katika kuhamasisha jamii juu ya huduma za ZBS kwa kutumia vyombo vya habari, bonanza na mitandao ya kijamii.

### 11.0.2 WAKALA WA USAJILI BIASHARA NA MALI ZANZIBAR (BPRA)

**66. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 BPRA ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 3.93** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 BPRA ilipanga kutumia **shilingi bilioni 2.96** hadi kufikia Machi, 2025

jumla ya **Shilingi bilioni 2.08** zimetumika sawa na asilimia 70. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 761.79** ziliingizwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi milioni 959.65** ziliingizwa kwa ajili ya mishahara na **Shilingi milioni 360.0** ziliingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, BPRA kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi bilioni 3.80** hadi kufikia Machi 2025, BPRA imeweza kukusanya **Shilingi bilioni 2.54** sawa na asilimia 66.8 ya makadirio.

**67. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025 BPRA imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Usajili wa Kampuni 1,109; Majina ya Biashara 1565; Alama za Biashara 1,023; na Nyaraka 8,540 vimefanyika.

ii. Wizara imefanya maboresho ya mifumo ikiwemo mfumo wa ORS na tovuti ya Ofisi pamoja na kujifunza maswali ya mifumo nchini Kenya. Aidha, nyaraka za usimamizi wa mifumo zimeandaliwa kwa lengo la kuweka udhibiti wa matumizi ya mifumo na vifaa vyote vya Tehama, "renewal of software license";

iii. Mapitio ya Sheria ya Ubia, Sheria ya Ufilisi, Sheria ya Wakala wa Usajili Biashara na Mali, Kanuni ya Mmiliki Mnufaika na tozo za Kanuni za Usajili wa Biashara na Mali yamefanyika;

iv. Elimu ya Usajili wa Biashara na Mali imetolewa kwa Masheha, Madiwani, Wakurugenzi wa Manispaa, Mabaraza na Halmashauri, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, elimu imetolewa kwa wananchi na wadau mbalimbali kupitia Tamasha la 11 la Biashara ya Kimataifa, Maonyesho ya sabasaba ambayo yalifanyika Dar es Salaam, Maonyesho ya Nane Nane na maonesho ya Fahari ya Zanzibar;

v. Elimu ya juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara na fursa zilizopo imetolewa kwa Wajasiriamali Wadogo Wadogo na wa Kati;

vi. Wafanyakazi 21 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mmoja (1) ya muda mrefu katika ngazi ya uzamili fani ya Uongozi wa Rasilimali watu;na

vii. BPRA imetoa mafunzo ya muda mfupi ya Zanmalipo, Qiuckbook na mafunzo ya Mfumo wa Usajili wa Mali Ubunifu kwa wafanyakazi 21 na mafunzo ya muda mrefu kwa mfanyakazi mmoja katika ngazi ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Uongozi wa Rasilimali watu katika Chuo cha Open University of Tanzania. Aidha, wafanyakazi wote wa BPRA wamepatiwa mafunzo ya huduma kwa wateja (Customer care service), mafunzo ya "Risk Assessment on Legal Person and Other Arrangements" yaliyofanyika Zanzibar kwa kushirikiana na GIZ kutoka nchini Ujerumani.

### 11.0.3 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

68. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika (Corporate Strategic Plan) wa miaka mitatu 2023-2025 pamoja na Mpango wa Biashara wa miaka mitano 2021-2025.

69. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2024/2025, Shirika lilikabiliwa na msimu mdogo wa vuno la karafuu. Hata hivyo, Shirika liliendelea kuimarisha bidhaa inazozizalisha na kuimarisha Majengo kwa lengo la kuongeza kipato na kuhuisha ustawi wa Shirika kwa kuhakikisha kwamba mashirikiano na Wadau wa zao la karafuu na bidhaa nyengine yanaimarishwa.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Baada ya Shirika kufanya mapitio ya bajeti yake kutokana na kushuka kwa uzalishaji wa karafu,lilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 43.57** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za Maendeleo, hadi kufikia Machi, 2024 Shirika limetumia jumla ya **Shilingi bilioni 12.64** sawa na asilimia 35 ya makadirio kwa miezi tisa. Aidha Shirika lilipanga kukusanya mapato ya **Shilingi bilioni 43.57** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo **Shilingi bilioni 39.59** zilikadiriwa kukusanywa na Shirika kwa miezi 9 kutokana na vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia Machi, 2025 ZSTC imeweza

kukusanya **Shilingi bilioni 9.54** sawa na asilimia 24.10 ya makadirio ya miezi tisa .

**71. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025 ZSTC imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Shirika katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 lilikadiria kununua tani 1,255 za karafuu kavu kwa gharama ya Shilingi bilioni 19.84. Hadi kufikia Machi 2025, Shirika limeweza kununua tani 412.4 za karafuu kavu kutoka kwa Wakulima kwa gharama ya Shilingi bilioni 6.24. Karafuu zilizonunuliwa sawa na asilimia 28.8 ya makadirio ya mwaka mzima;

ii. Shirika lilikadiria kununua jumla ya tani 255 za makonyo kwa gharama ya Shilingi milioni 401.6 Hadi kufikia Machi 2025, Shirika limenunua jumla ya tani 5.9 za makonyo kwa gharama ya Shilingi milioni 8.85 sawa na asilimia 2.31 ya makadirio kwa miezi tisa (9), kwa kawaida ununuzi wa makonyo huongezeka baada ya kukamilika kwa msimu wa ununuzi wa karafuu. Aidha, manunuzi ya karafuu pamoja na makonyo yamepungua kutokana na msimu kuwa mdogo kinyume na matarajio ambapo umesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi. Shirika limenunua kilo moja ya karafuu kwa bei ya 15,000 kwa daraja la kwanza, daraja pili Shilingi 13,500 , daraja la tatu Shilingi

12,500 na mpeta Shilingi 7,000 kutoka kwa mwananchi;

iii. Shirika limefanikiwa kuuza karafuu nje ya nchi kwa bei ya USD 6,650 kwa tani moja FOB Zanzibar na makonyo yameuzwa kwa bei ya USD 930 kwa tani moja FOB Zanzibar. Aidha, Shirika limeweza kuuza nje ya nchi jumla ya tani 412.4 za karafuu, tani 8 za makonyo na tani 150 za unga wa makonyo ambao uliuzwa kwa shilingi 218.6 milioni.;

iv. Katika kuimarisha uzalishaji wa zao la karafuu Shirika limenunua miche 32,000 ya mikarafuu na kupatiwa wakulima Unguja na Pemba. Aidha Shirika linaendelea kushirikiana na chuo cha mafunzo katika kuanzisha mashamba ya mikarafuu pamoja na kuanzisha Vitalu vya kuotesha miche ya mikarafuu;

v. Shirika pia limeendelea kushirikiana na Kikosi cha kupambana na Magendo na wananchi wema ili kupata taarifa za usafirishaji wa magendo ya Karafuu;

vi. Pia Shirika lilisimamia malipo ya bima kwa wakulima 81 walioanguka mwaka 2023/2024, ambapo kati ya hao wakulima 69 wamelipwa shilingi 97.9 milioni na wakulima 12 wanaendelea kufuatiliwa malipo yao.

vii. Katika kuhakikisha uwepo wa mfumo mzuri wa kuendeleza zao la karafuu Shirika lilizindua zoezi la kufanya usajili wa kuwatambua wananchi wenye mashamba ya mikarafuu kwa ngazi za Shehia ambapo hadi tarehe 31, Machi 2025 Shirika liliweza kusajili wakulima 6,458 na mashamba 12,784 katika Wilaya za Mkoani, Chake - Chake na Wete.

### 11.0.4 KAMPUNI YA MWANI (ZASCO)

**72. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kampuni ya Mwani ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 8.30 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi bilioni 1.04 zimetumika sawa na asilimia 12.63.

**73. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Kampuni imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

i. Wizara inatarajia kufunga mashine katika Kiwanda cha Kusarifu Mwani Chamanangwe ambapo imeingia Mkataba na Kampuni ya Nutri-san. Mpaka sasa Mikataba kwa ajili ya kufanikisha upatikanaji wa mashine hizo imeshatiwa saini baina ya Kampuni ya Nutri-san (mbia katika kiwanda) na Kampuni ya Mitsubishi. Aidha mashine hizo zinatarajiwa kutoka nchini Japan katika Kampuni hiyo;

ii. Kampuni imenunua wastani wa tani 824.6 za Mwani. Kati ya hizo, tani 619.5 ni mwani aina ya "Spinosum", tani 48.6 mwani aina ya "Cottonii" na tani 198.2 za mwani aina ya Ulva;

iii. Kampuni imeuza tani 188 za Mwani mkavu nchini Vietnam na China. Kati ya hizo, tani 163 ni mwani aina ya Ulva na tani 25 ni mwani aina ya "Spinosum";

iv. Kampuni imeshiriki maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika Dole, Mkoa wa Mjini Magharibi na Maonesho ya siku ya Chakula Duniani Chamanangwe - Pemba. Aidha, Kampuni ilishiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar. Kupitia maonesho hayo, Kampuni imeweza kujitangaza kwa washiriki mbali mbali wa maonesho hayo;

v. Kampuni imetoa mafunzo juu ya mbinu bora za kulima mwani kwa wakulima wa mwani. Aidha, mafunzo ya umuhimu wa kutumia huduma za kibenki katika kuhifadhi fedha za wakulima wa mwani imetolewa kwa wakulima 200 Unguja na 150 Pemba; na

vi. Shughuli mbali mbali za Kampuni kwa upande wa Pemba zimeratibiwa na kusimamiwa. Shughuli hizo ni pamoja na ununuzi wa mwani wa "Spinosum" na "Cottonii" pamoja na ugawaji wa vifaa kwa wakulima wa mwani.

## 12.0 MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 12.0.1 Vipaumbele Vya Wizara Na Taasisi Zake Kwa Mwaka 2025-2026.

74. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutayarisha bajeti ya mwaka 2025/26, Wizara imezingatia nyenzo muhimu ambazo ni Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Hotuba na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ushauri wa Baraza la Wawakilishi na Miongozo mbalimbali ya Kisera na Kisheria inayosimamiwa na Wizara.

75. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza vipaumbele katika maeneo makuu matatu (3) ambayo yanalenga kuimarisha Sekta ya viwanda, kuimarisha Biashara na kutafuta Masoko pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na utoaji huduma. Maeneo hayo ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo:-

### 12.0.2 Sekta Ya Viwanda

76. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza sekta ya Viwanda, Wizara ya Biashara na Maendeleo

ya Viwanda kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 imepanga **Kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda Dunga, Chamanangwe na Pangatupu.** Kwa upande wa Dunga Wizara inatarajia kuweka miundombinu ya jengo la Utawala na majengo ya Viwanda na kwa upande wa Chamanangwe Wizara inatarajia kuweka miundombinu ya majengo ya Viwanda, Maji, Umeme pamoja na Barabara za ndani. Aidha, upande wa Pangatupu Wizara imepanga kufanya upimaji wa udongo na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi.

### 12.0.3 Sekta ya Biashara

Kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Biashara, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2025/2026 imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. **Kuendeleza Ujenzi kwenye eneo la Kituo cha maonesho ya kibiashara Dimani** kwa kuendelea kuimarisha miundombinu tofauti ikiwemo kujenga ghala la kuhifadhia vifaa, kuimarisha jengo la kuuzia chakula, kuweka miundombinu ya eneo la kufurahishia watoto pamoja na kuuimarisha ukumbi wa mikutano kuwa na vifaa vya kisasa vitakavyowezesha Mikutano mikubwa ya Kimataifa kufanyika.

ii. **Kuratibu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre):** Wizara itaendelea

na juhudi za kutafuta Wawekezaji wenye masharti nafuu ili kushirikiana katika ujenzi wa Kituo hiki. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Exim ya Jamhuri ya Korea imepanga kufanya Upembuzi Yakinifu wa kituo hicho ambapo Mshauri Elekezi anatarajiwa kuanza kazi hiyo kuanzia mwezi Juni 2025 hadi Disemba 2025 katika eneo la ujenzi wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano.

### 12.0.4 Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Huduma

**78. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Mazingira ya ufanyaji Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kufanya mapitio ya Sheria ya Biashara pamoja na Kanuni zake;

ii. Kuendelea na mazungumzo na kutatua changamoto za kibiashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara;

iii. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa matokeo ya Ripoti ya Tathmini ya Kuimarisha Mazingira ya Kibiashara kwa lengo la kuimarisha mazingira ya Biashara na Uwekezaji;

iv. Kuratibu Uandaaji wa Mkakati wa Mauzo ya Nje ya Zanzibar (Zanzibar Export Strategy);

v. Kuandaa Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Leseni;

vi. Kuandaa Kanuni ya Sheria mpya Nambari moja (1) ya mwaka 2025 ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni;

vii. Kusimamia na kukuza tasnia ya Hakimiliki kibiashara (Management and Commercialization of Copyright Industry);

viii. Kufanya mapitio ya Sheria ya Hakimiliki (Namba 14) ya mwaka 2003 kwa lengo la kuimarisha usimamizi na ulinzi wa hakimiliki; na

ix. Kuimarisha mfumo wa taarifa wa uendeshaji wa Mashauri ya Rufaa.

### 12.0.5 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

**79. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza Taasisi ya Viwango, kwa mwaka 2025/2026 Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuweka mfumo wa TEHAMA utakaofanikisha mifumo na utekelezaji wa kazi za ZBS na mifumo ya ukusanyaji wa mapato;

ii. Kupata Ithibati ( Accreditation) ya Maabara tano (5) ambazo ni Maabara ya Nishati, Nguo na Ngozi, Vifungashio, Chakula na Vimelea kwa ktumia Kiwango cha Maabara ISO/IEC 17025:2017;

iii. Kuwekeza katika Maabara ya Kemikali, Nishati, Chakula, Upimaji wa Gesi, Kituo cha kuhifadhia data pamoja na ununuzi wa vifaa vya Maabara (Phase- 2);

iv. Kufanya ujenzi wa Maabara ya Nishati ya mafuta, Pemba;

v. Kuanza mchakato wa ujenzi wa Afisi ya Uratibu Pemba; na

vi. Kuweka Mfumo wa Miundombinu ya Teknologia na Kielektroniki katika kurahisisha utoaji wa huduma za Taasisi.

### 12.0.6 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA)

80. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali kwa mwaka 2025/2026 imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imepanga kufanya maboresho na kuongeza mifumo ya usajili wa mali na biashara.

ii. Kuboresha na kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili na kuhifadhi nyaraka (kumbukumbu).

### 12.0.7 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

81. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara kupitia Shirika itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kutanua Wigo wa ununuzi wa Karafuu kwa kuanza kununua Karafuu kutoka katika Mikoa ya Tanzania bara pamoja na kuendelea na kununua karafuu hapa Zanzibar;

ii. Uzalishaji wa Vifungashio vya Bidhaa mbali mbali hasa bidhaa za karafuu na mazao mengine ya kilimo;

iii. Kutanua wigo wa Biashara zinazoendeshwa na ZSTC kwa kuanza kufanya biashara ya Bidhaa za Vyakula muhimu hapa Zanzibar;

iv. Kuendelea na kufanya Uwekezaji majengo ya Vitega uchumi (Real Estate Investments); na

v. Kuendeleza viwanda vya uzalishaji wa mafuta ya mimea.

### 12.0.8 KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR (ZASCO)

**82. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Kampuni ya Mwani itatekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuanza uzalishaji katika Kiwanda cha kusarifu mwani Chamanangwe Pemba.

ii. Kuimarisha uwezo wa wakulima juu ya kuandaa mwani baada ya uvunaji.

iii. Kutafuta Masoko mapya ya mwani kwa kufanya Utafiti wa soko la mwani kwa bidhaa mahsusi ikiwemo bidhaa za mwani, vipodozi vyakula vya mifugo, mbolea na rangi za chakula.

## 13.0 MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/2026

**83. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha

2025/26 imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 57.55.** Kati ya fedha hizo jumla **Shilingi bilioni 1.96** kwa Matumizi ya kazi za kawaida na **Shilingi bilioni 3.47** kwa malipo ya mishahara. Aidha, **Shilingi bilioni 46.36** zimetengwa kwa kazi za Maendeleo kwa Programu ya kuendeleza maeneo ya Viwanda na Mazingira Bora ya Biashara. Aidha, Wizara imepangiwa Shilingi bilioni 5.75 kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kwa Taasisi za Wizara.

**84. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda itatekeleza Programu Kuu tatu (3). Programu kuu hizo ni programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali; na Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara.

**85. Mheshimiwa Spika,** Katika programu kuu ya kwanza ambayo ni Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; imegawika katika Programu ndogo tatu (3). Program hizo ni Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara kwa Pemba. Katika kutekeleza shughuli zake, programu hii imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 4.52**

**86. Mheshimiwa Spika,** Katika Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na

Utumishi. Katika kutekeleza majukumu yake programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 2.95**

87. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la uandaaji na uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda. Katika kutekeleza majukumu yake programu hii imepangiwa **Shilingi milioni 482.5**

88. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo inaratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 1.08**

89. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya pili ambayo ni Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali imegawika katika Programu ndogo mbili. Program hizo ndogo ni Ukuzaji Viwanda na Maendeleo ya Ujasiriamali. Katika kutekeleza shughuli za programu hii imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 36.01**

90. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda ina jukumu la kutoa huduma ya uimarishaji wa Sekta ya Viwanda, Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's na Ukuzaji wa MSME's. Ili kutekeleza

majukumu yake programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 35.98**

91. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ambayo ina jukumu la kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali ili kutekeleza programu hii ndogo imepangiwa **Shilingi millioni 32.01**

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya tatu ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Programu hii imegawika katika Programu ndogo tatu (3) ambazo ni Ukuzaji masoko na usafirishaji; uwezeshaji biashara na utengamano wa kibiashara. Ili kutekeleza huduma zilizopangwa katika Programu kuu hii kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 17.02**

93. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji ina jukumu la kutoa huduma ya kuongeza fursa za masoko kwa bidhaa za Zanzibar pamoja na urahisisishaji biashara. Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji imepangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 11.13**

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara yenye jukumu la kuimarisha mazingira mazuri ya biashara ambayo inatekelezwa na Idara ya Biashara, pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ambazo ni ZFCC, BLRA, ZAWEMA, COSOZA, ZNBC na ZFCT. Ili kutekeleza jukumu lake kupitia programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 5.82**

95. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara wenye jukumu la kuimarisha biashara huria inayopelekea upanuzi wa soko na kuongeza biashara baina ya nchi na nchi itasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza shughuli zilizopangwa programu hii ndogo imepangiwa jumla ya **Shilingi milioni 59.78**

## 14.0 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 14.0.1 MAPATO YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/2026

96. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara yangu imepangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi billioni 3.51** ukilinganisha na makusanyo ya mwaka 2024/2025 ya **Shilingi Bilioni 1.93** Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio kama inavyoonekana katika **Jadweli Nambari 1.**

### Jadweli Nambari 1: Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

| KIFUNGU | MAELEZO | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **1,025,436,800** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 1,025,436,800 |
| | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **1,741,788,040** |
| 1422077 | Malipo ya kazi za Biashara | 1,741,788,040 |
| | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **43,635,609** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 43,635,609 |
| | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRA)** | **91,162,059** |
| | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **181,693,219** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 181,693,219 |
| | | |
| **R0101** | **Afisi kuu Pemba** | **72,211,478** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 72,211,478 |
| | | |
| **R0114** | **Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki** | **363,742,796** |
| 1422117 | Mapato ya usajili na ada ya Mwaka | 363,742,796 |
| **JUMLA KUU** | | **3,519,670,000** |

## 14.0.2 MATUMIZI KWA MWAKA 2025/2026

97. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2025/26 imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni 57.55 Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 46.36 zimepangwa kwa ajili ya kazi za Maendeleo, Shilingi bilioni 1.96 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi bilioni 3.48 kwa ajili ya mishahara. Aidha, Shilingi bilioni 5.75 zimepangwa kwa ajili ya ruzuku

ya mishahara na kazi za kawaida kwa Taasisi za Wizara. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali nambari 2.**

**Jadweli Nambari 2: Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2025/2026**

| KIFUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na uratibu wa Wizara BMV** | 4,520,569,000 |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 2,956,524,000 |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara | 482,520,000 |
| SR010103 | Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 1,081,525,000 |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **36,012,784,000** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 35,980,770,000 |
| SR010202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 32,014,000 |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **17,021,117,000** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 11,137,729,000 |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 5,823,608,000 |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 59,780,000 |
| **JUMLA YA KIFUNGU R01** | | **57,554,470,000** |

## 15.0 HITIMISHO

98. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia maelezo ya Hotuba hii napenda kukushukuru tena wewe binafsi, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni** na Wajumbe wote wa Kamati na Makatibu wa Kamati hiyo kwa kushirikiana na Wizara pamoja na kutupatia maoni na ushauri ambayo yametusaidia kwa kiasi kikubwa kuleta maendeleo katika Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini.

99. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa wale wote walioshirikiana nasi kufanikisha malengo ya Wizara katika kipindi cha mwaka 2024/2025 miongoni mwao ni Wizara ya Biashara na Viwanda ya Tanzania Bara, Trade Mark Africa (TMA),Tan Trade, Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Malibunifu Duniani (WIPO), Shirika la Miliki Bunifu Kanda ya Afrika ( ARIPO), Kampuni ya YAS, AZAM, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Benki ya CRDB, REPOA, TECHNO SAVE Jumuiya ya Wafanyabiashara (ZNCC), ZIPA, Shirika la Utangazaji Zanzibar, ZICTIA na

Wafanyabiashara na Wajasiriamali mbali mbali waliosaidia Wizara pamoja na Washirika wengine ambao sikuweza kuwataja hapa leo.

100. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda niwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda nikianza na Katibu Mkuu Ndugu Fatma Mabrouk Khamis, Naibu Katibu Mkuu Dkt Said Seif Mzee, Wakuu wa Taasisi wote, Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa mashirikiano yao wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ni matarajio yangu kwamba mashirikiano hayo yataendelezwa kwa ufanisi zaidi katika mwaka wa fedha 2025/2026 ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

101. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini si kwa umuhimu,napenda kutoa shukuran zangu za dhati kwa familia yangu yote, kwa upendo na utulivu wa nafsi wanayonipatia katika kipindi chote ninapokuwa kwenye majukumu mazito ya kitaifa. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwalipa upendo wa kuwajibika kama Baba, Mume na Mlezi wa Familia.

102. **Mheshimiwa Spika,** Siwezi kumaliza hotuba yangu hii bila ya kuwashukuru kwa dhati viongozi na wanachana wenzangu wa Chama cha ACT Wazalendo wa ngazi zote kwa imani yao kubwa kwangu na malezi ya kisiasa wanayonipatia. Niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwa mwanachama mtiifu na

muaminifu hadi pale dhamira na malengo ya Chama yatakapotimia.

103. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya taarifa hii, naomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kupokea, kujadili na hatimae kuikubali taarifa hii ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 na kuidhinisha makadirio ya Shilingi bilioni 57.55 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

104. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



..................................

**MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN**

**WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA ZANZIBAR.**

# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho Nambari 1:

## Uwepo wa Bidhaa muhimu za chakula Kwa kipindi cha Julai, 2024 - Machi, 2025.

| Bidhaa/Kutoka | Bidhaa/tani | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mchele | Sukari | Unga wa ngano | Mafuta ya kupikia |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka Nje ya Nchi (Julai-Machi) | 24,746.08 | 18,708.02 | 705.50 | 102,207.71 |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka T. Bara (Julai-Machi) | 2,538.90 | - | 1,912.85 | - |
| Bidhaa Zilizozalishwa nchini (Julai-Machi) | - | 7,900.00 | 56,723.76 | - |
| **Jumla ya Bidhaa** | **27,284.98** | **26,608.02** | **59,342.11** | **102,207.71** |

## Kiambatanisho Nambari 2:

## Wastani wa bei za Jumla na Reja Reja kwa Mwezi wa Julai 2024 hadi Machi, 2025 katika soko

| BIDHAA | Bei za Jumla | | Bei za Reja Reja | |
|---|---|---|---|---|
| | Thamani | Ujazo | Thamani | Ujazo |
| Sukari | 104,000-125,000 | 50 Kg | 2,200-2,800 | 1 Kg |
| Mchele | 79,000-103,000 | 50 Kg | 1,800-2,200 | 1 Kg |
| U/Ngano | 65,000-78,000 | 50 Kg | 1,600-2,000 | 1 Kg |
| Mafuta ya Kupikia | 75,000-81,000 | 20 Litres | 5,000-9,500 | 1.5 Litres |
| Saruji | 15,000-16500 | 50 Kg | 16,500-17,000 | 50 Kg |

**Kiambatanisho Nambari 3:**

## Mapato ya Wizara kwa kipindi cha Miezi Tisa Mwaka wa Fedha 2024/2025

| Kifungu | Maelezo | Makadirio kwa Mwaka 2024/25 | Makadirio kwa Miezi Tisa 2024/25 | Makusanyo kwa Miezi Tisa 2024/25 | Asilimia ya Makusanyo Kwa miezi Tisa |
|---|---|---|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **564,000,000** | **441,557,000** | **249,473,271** | **56%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 564,000,000 | 441,557,000 | 249,473,271 | 56% |
| | | | | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **958,000,000** | **710,000,000** | **689,801,000** | **97%** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 958,000,000 | 710,000,000 | 689,801,000 | 97% |
| | | | | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **14,000,000** | **14,000,000** | **19,543,473** | **140%** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 14,000,000 | 14,000,000 | 19,543,473 | 140% |
| | | | | | |
| **R0110** | **Mamlaka ya Leseni (BLRA)** | **50,140,000** | **48,000,,000** | **5,048,728** | **11%** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa Mamlaka za Leseni | 50,140,000 | 48,000,000 | 5,048,728 | 11% |
| | | | | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **99,933,000** | **72,247,000** | **62,170,000** | **86%** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 99,933,000 | 72,247,000 | 62,170,000 | 86% |
| | | | | | |
| **R0114** | **Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki** | **200,062,000** | **180,000,000** | **151,317,400** | **84%** |
| 1422117 | Mapato ya usajili na Ada ya Mwaka | 200,062,000 | 180,000,000 | 151,317,400 | 84% |
| | | | | | |
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **49,717,000** | **37,448,500** | **32,558,691** | **81%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 39,717,000 | 32,807,000 | 27,658,691 | 84% |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 10,000,000 | 7,500,000 | 4,900,000 | 65% |
| **Jumla Kuu** | | **1,935,852,000** | **1,506,111,000** | **1,209,912,563** | **80%** |

**Kiambatanisho Nambari 4:**

**Mchanganuo wa matumizi ya fedha kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi), 2024/2025**

| FUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | KIASI KILICHOPANGWA KWA MWAKA | MAKADIRIO KWA MIEZI TISA | MATUMIZI KWA MIEZI TISA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biasharara na Maendeleo ya Viwanda** | **3,863,419,798** | **2,985,823,123.00** | **2,505,994,343.67** | **83.9** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 2,237,335,998 | 1,715,135,273.00 | 1,630,126,189.43 | 95.0 |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara | 522,766,900 | 414,709,175.00 | 254,651,453.24 | 61.4 |
| SR010103 | Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 1,103,316,900 | 855,978,675.00 | 621,216,701.00 | 72.6 |
| | | | | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **40,759,520,776** | **40,654,035,582.00** | **11,245,812,055.94** | **27.7** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 40,725,968,776 | 40,631,608,582.00 | 11,245,812,055.94 | 27.7 |
| SR010202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 33,552,000 | 22,427,000.00 | - | 0.0 |
| | | | | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **15,658,059,426** | **14,390,867,562.01** | **4,655,466,027.61** | **32.4** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 10,368,346,426 | 10,244,696,562.00 | 1,840,821,346.90 | 18.0 |
| SR010305 | Uwezeshaji wa Biashara | 5,245,873,000 | 4,113,651,000.01 | 2,805,619,680.71 | 68.2 |
| SR010306 | Utengamano wa Biashara | 43,840,000 | 32,520,000.00 | 9,025,000.00 | 27.8 |
| **JUMLA YA KIFUNGU RO1** | | **60,281,000,000** | **58,030,726,267.01** | **18,407,272,427.22** | **31.7** |

## Kiambatanisho Nambari 5.

**Kampuni zilizopewa hati za ujenzi wa viwanda Dunga Zuze**

| SN | Jina la kampuni | Bidhaa | Asili ya Mmiliki |
|---|---|---|---|
| 1. | Mama Afrika | Khanga na Kitenge | Uingereza |
| 2. | Africa Bio Chem Pharma | Dawa za magonjwa ya binaadamu na Chanjo | China |
| 3. | SK Medicines DMCC | Dawa za magonjwa ya binaadamu | India |
| 4. | Elaf Metal Company | Usarifu wa chuma chakavu (metal recycling) | Pakistan |
| 5. | Eco Pro | Usarifu wa Plastiki (plastic recycling) | Tanzania |
| 6. | Hakam Investment Limited | Nondo, Waya na Misumari | Tanzania |
| 7. | Solar Tribe Tanzania | Vyombo vya moto vinavyotumia nishati ya Jua | Tanzania |